
# KANISA
# LA MAHALA PAMOJA



Pastor James Kalekwa

# KANISA LA MAHALA PAMOJA

James Kalekwa

# Orodha ya Yaliyomo

Tabaruku ........................................................................ 4

Salamu na Utangulizi ........................................................... 5

SURA YA KWANZA: ........................................................ 7

TABIA YA MAFUNDISHO YA NENO LA MUNGU ........ 7

SURA YA PILI: ..................................................................29

USHIRIKA WA KANISA LA MAHALA PAMOJA...........29

SURA YA TATU: UTOAJI WA KUJIDHABIHU ..............43

Madaraja matatu ya utoaji:..............................................44

i. Utoaji kumuelekea Bwana ........................................44

ii. Utoaji kuielekea kazi ya Bwana. ...............................48

iii. Utoaji kumuelekea mtumishi wa Mungu...............52

Dhana ya Upimaji wa Sadaka. .........................................54

Pande mbili pacha za muamala wa sadaka. .......................55

SURA YA NNE:.................................................................57

UTARATIBU NA NIDHAMU YA WAAMINI...................57

Nani ananufaika na suala la nidhamu na utaratibu? ..........63

Kwa nini tuonyeshe usimamizi wa nidhamu ya kanisa? ...66

Kuhusu Mwandishi:...........................................................67

Kuhusu New Vine Church:..................................................67

Mawasiliano na Mwandishi: ................................................68

# Tabaruku

Mfululizo wa vitabu hivi vya kieltroniki (e-books) bure kwa kila atakaye; ni himizo la kiungu ndani yangu kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari.

Ninatabaruku kitabu hiki kwa kanisa la Kristo na kwa nchi yangu niipendayo, Tanzania.

Kanisa litashinda na kushamiri zaidi!

Tanzania, ninakupenda kwa moyo wote!

## Salamu na Utangulizi

Mfululizo huu wa vitabu vya kieletroniki ni maono ambayo Mungu ameweka ndani ya mtumishi wake, mume wangu mpenzi, kama namna yake ya kuonyesha shukurani kwa Mungu kwa zawadi ya maisha.

Ninamfahamu mume wangu kama mtu anayempenda Mungu kupitiliza. Yuko tayari kulipia gharama yoyote ile kuonyesha hilo. Ni mtu anayewapenda watu wa Mungu kwa namna ambayo sijawahi kuona. Yamekuwa ni maombi yake kuyagusa maisha ya wengi kwa kadiri inavyowezekana kabla Yesu Kristo hajarudi.

Anapoadhimisha siku ya kuzaliwa kwake **Juni 20**, amekuandikia kitabu hiki, akapangilia na kufanya kipatikane kwako bila malipo yoyote. Nimemwona anavyokesha; wakati mwingine kuamka alfajiri sana au kuchelewa sana kulala ili kukamilisha uandishi. Nimemuona anavyoomba na kuombea wasomaji, anavyojisomea na kutafiti ili kuhakikisha anafanya uwasilishaji wa thamani.

Ningependa tuthamini zawadi hii ambayo sisi wengine tunanufaika nayo bila kulipia gharama:

1. Mshukuru Mungu pamoja nasi kwa zawadi hii ya maisha ya Pastor James Kalekwa kisha muombee maisha marefu na afya njema.

2. Mwandikie ujumbe wa kumsalimu na kumpongeza ukisema ni kwa namna gani huduma yake imeyagusa maisha yako. Ninajua hili litaufurahisha sana moyo wake.
3. Wafikishie vitabu hivi walau watu hamsini tu. Ni vitabu vinatolewa bila malipo (vimeyagharimu maisha ya mwandishi ili vikufikie).
4. Usiuze vitabu hivi. Tuligundua kuwa kuna watu wanavisambaza kwa malipo ya fedha. Hiyo si sawa. Itakuwa ni kwa hasara yako mwenyewe ukifanya hivyo.

Baada ya kuyasema hayo, nikuhakikishie ya kwamba mtu huyu mkuu wa Mungu amejaa hekima za kiungu na neno ambalo siku zote hutokeza shuhuda maishani mwa wengi. Kwa kusoma kitabu hiki, ushuhuda wako unafuatia. Nikutakie usomaji mwema.

Na heri ya kuzaliwa kwa mpendwa wetu, zawadi ya mbingu kwenye kizazi chetu, Pastor JK.

Frida James Kalekwa (Mama Pastor JK)
Mke wa mwandishi
Juni, 2024
Dodoma, Tanzania

# SURA YA KWANZA:

# TABIA YA MAFUNDISHO YA NENO LA MUNGU

Mathayo 16:18, *"Nami nakuambia, wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda."*

Yesu anapolijenga kanisa analijenga kwa ukuaji wa kiidadi, ukuaji wa kijiografia (kuenea/kusambaa) na ki ushawishi (influence). Na kanisa linapokuwa likijengwa, linajengwa kuyaelekea malango ya kuzimu. Ujenzi wake hauna maana ya kuwa limebaki sehemu moja (rigid/static), bali kanisa linajengwa kwa hali ya uendelevu. Hivyo, malango ya kuzimu ni kama yanajitetea au kujilinda dhidi ya kanisa; wakati huo kanisa linasonga mbele kwa kushambulia. Yaani, kanisa ni *offensive* kwa asili wakati malango ya kuzimu ni *defensive!* Habari njema ni kuwa kanisa litapenya katikati ya kila aina ya mashindano.

Kanisa ni mali ya Bwana Yesu na wala si mali ya mtu yeyote yule. Kwa sababu hiyo basi, yeye ndiye anayo ramani nzima ya ujenzi wa kanisa lake, na sisi wengine tunaongoza na kufuata chini ya ramani yake. Hivyo ni vizuri kujua kuwa chochote kinachofanywa ndani ya kanisa (kiwe kizuri ama kibaya) kinafanywa kumuelekea mwenye kanisa ambaye ni Bwana Yesu mwenyewe.

Nilifundishwa jambo hili mapema sana na baba yangu wa kiroho, mtumishi wa Mungu, Bishop Goodluck Kyara, ya kwamba Yesu ndiye mmiliki na mjenzi wa kanisa. Kwa faida ya kila mtumishi atakayesoma hapa. Uelewa huu ukiingia moyo na ukautendea kazi kwa dhati kabisa. Utapunguza mateso yasiyo ya lazima kwenye utumishi na kazi ya Mungu.

Kanisa la mahala pamoja lenye nguvu ni kanisa ambalo limejengwa kwenye msingi wa Neno la MUNGU. Washirika wa kanisa la mahala pamoja lenye nguvu ni watu ambao wanapenda kusikia mafundisho ya Neno la

Mungu. Ukiwaondolea mafundisho, umewaondolea nguvu zao.

Hebu tuangalie jinsi kanisa la mwanzo kabisa, kanisa la Matendo ya Mitume la pale jijini Yerusalemu. Ni vyema ukafahamu ya kwamba kanisa hili lilifahamika kama, *"Wale walioupindua ulimwengu"* (Mdo 17:6); Kanisa hili lilishutumiwa ya kuwa *"wameijaza Yersulaemu kwa mafundisho yao"* (Mdo 5:28) – Si unafahamu Yerusalemu ni jiji kubwa lililokuwa linakusanya watu wa dunia nzima (ni kama vile kusema jiji la New York. Au kwa muktadha wetu wa Tanzania jiji la Dar es Salaam – mahala ambapo watanzania wa kabila zote utawakuta). Fikiria kanisa moja limeujaza mji kwa mafundisho… siyo jambo dogo hilo.

Kumbuka kanisa hilo lilikuwa na wahudumu wa mezani ambao walikuwa na uelewa mkubwa sana wa kimafundisho na mtembeo wa nguvu za Mungu. Unamkumbuka Stefano na Filipo. Kwa taarifa yako hao ni wahudumu wa mezani tu (Mashemasi) – Rejea Mdo 6:5

Kuhusu Stefano rejea: Mdo 6:8-10/7:54-60

Kuhusu Filipo rejea: Mdo 8:4-8, 26-40

Hili kanisa lenye watumishi wa namna hii; Kanisa lenye washirika wa namna hii; Lilikuwa na tabia gani; Chanzo chake cha nguvu kilikuwa ni nini hasa?

Matendo 2:42, *"Wakawa* ***wakidumu katika fundisho la mitume****, na katika ushirika, na katika kuumega mkate na katika kusali."*

Kanisa la mwanzo hawakuwa na vitu vya kutisha sana kwa namna ya mwilini bali walikuwa na matokeo makubwa yaliyowatisha wafalme na watu wenye nguvu. Tabia hii ndiyo iliyowapa nguvu.  Kwao, mafundisho yalikuwa ni kipaumbele chao na waliifanya tabia hii kwa uendelevu, mafundisho ya Neno la Mungu haikuwa ni tendo la mara moja. Walikuwa wakidumu!

Haiwezekani kutenganisha maisha yao ya siku kwa siku na fundisho la Neno la Mungu.

Mathayo 28:19-20, *"Basi, enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu;* ***na kuwafundisha yote***

*niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote hata ukamilifu wa Dahari."*

Agizo kuu halijakamilika kama mafundisho hayajafanyika. Yaani utekelezaji na ukamilishaji wa agizo kuu unahusisha mafundisho ya neno la Mungu kwa uedelevu ndani ya kanisa.

Kwa hiyo, mafundisho ya neno la Mungu ndiyo shughuli ya kanisa la mahala pamoja. Hebu nikutazamishe maandiko kadhaa hapa yatufae kufanya tafakari ya kina.

Waefeso 4:11-15, *"Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii, na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu;* ***kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu****, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo;….."*

Waebrania 5:11-14, *"Ambaye tuna maneno mengi ya kunena katika habari zake; na ni shida kuyaeleza kwa kuwa mmekuwa wavivu kusikia. Kwa maana, iwapasapo*

*kuwa waalimu, (maana wakati mwingi umepita), mnahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu; nanyi mmekuwa mnahitaji maziwa wakla si chakula kigumu. Kwa maana kila mtu atumiaye maziwa hajui sana neno la haki, kwa kuwa ni mtoto mchanga. Lakini chakula kigumu ni cha watu wazima, ambao akili zao kwa kutumiwa, zimezoezwa kupambanua mema na mabaya."*

1 Wakorintho 3:1-2, *"Lakini ndugu zangu mimi sikuweza kusema nanyi kama na watu wenye tabia ya rohoni bali kama na wtu wenye tabia ya mwilini, kama na watoto wachanga katika Kristo. Naliwanywesha maziwa, sikuwalisha chakula; kwa kuwa mlikuwa hamjakiweza. Naam, hata sasa hamkiwezi,"*

1 Yohana 2:12-14, *"Nawaandikia ninyi, watoto wadogo kwa sababu mmesamehewa dhambi zenu, kwa ajili ya jina lake. Nawaandikia ninyi, akina baba kwa sababu mmemjua yeye aliye tangu mwanzo. Nawaandikia ninyi, vijana, kwa sababu mmemshinda yule mwovu. Nimewaandikia ninyi, watoto, kwa sababu mmemjua Baba, Nimewaandikia ninyi, akina baba, kwa sababu*

*mmemjua yeye aliye tangu mwanzo. Nimewaandikia ninyi, vijana, kwa sababu mna nguvu, na neno la Mungu linakaa ndani yenu, nanyi mmemshinda yule mwovu."*

Mafundisho ya neno la Mungu yamekusudiwa kusababisha matokeo, na kuacha alama fulani ndani ya watu wanaosikiliza hayo mafundisho.

Kwa kutambua ya kwamba mtu anapookoka, anatambuliwa ya kwamba amezaliwa upya – ni kama ule mchakato wa ukuaji kwenye maisha ya kimwili kabisa. Kazi ya mafundisho ni kuwezesha makuzi ya mtoto huyu katika masiha ya kiroho.

Kanisa la mahala pamoja linalowekeza muda mwingi kwenye mafundisho litaona matokeo haya kwa ngazi ya pamoja na ngazi ya mshirika mmoja mmoja kwenye maisha yao ya siku kwa siku.

i. Ukuaji.

Watoto wachanga kiroho wana tabia ya kusamehewa dhambi na kumjua Baba, hawana mambo mengi.

Wameokoka hivi karibuni na ufahamu wao ni kuhusu mambo ya msingi. Na wao hata hivyo wameandikiwa ujumbe.

Vijana, wanazo nguvu na wana *"vurugu za kiroho"*. Hili ni kundi la watu wanaotaka kuthibitisha ukweli wa wanayojifunza. Wanao uwezo wa kuchokoza mambo ya kiimani kama vile afya na uponyaji wa kiungu, vita za kiroho… maadamu amekua anao uwezo wa kujisimamia wenyewe.

Wababa, ni kundi ambalo limekomaa kwa kuzoezwa elimu ya Mungu. Hawana tena mashaka kuhusu kweli za Biblia. Wana ujasiri sana na neno la Mungu na utendaji wake kwa namna ambayo huwezi kuwatikisa. Neno la Mungu limegeuka kuwa maisha yao ya siku kwa siku. Wamekuwa mapacha wanaofanana na neno… Yaani, unaweza ukawaona wao ukawa umeliona neno. Unaweza ukalisoma neno kisha ukawaona/ukawakumbuka wao kama miili inayolitekeleza neno hapa duniani na kwenye zama na kizazi husika

Lazima kuwe na ukuaji kutoka kwenye utoto wa kiroho kulekea ujana mpaka kufika kwenye kuwa baba katika hali ya kiroho. Ukuaji utaamua kanisa lifundishwe mafundisho ya aina gani.

Kanisa linalopenda mafundisho ni kanisa la watu wanaokua.

ii. Umoja wa Imani.

Kanisa lenye nguvu lina tabia ya kuwa na mfanano (commonness) kwenye kila eneo la maisha ambalo Biblia linatoa ufafanuzi mmoja. Kanisa ambalo lina mafundisho lina umoja wa kiimani kwenye kila eneo la maisha (holistically) wamejaa maandiko, na wanaamini kwa kufanana sawasawa na fundisho la ki Mungu.

Yesu ametuokoa na ametukusanya kutoka kila kabila, lugha, jamaa na taifa… ni kusema kila mmoja amekuja kutokea *background* tofauti. Hivyo, kuna falsafa, uelewa, mitazamo, misimamo, hisia… tuna tofautiana kwa namna nyingi sana na tofauti zetu nazo zinatofautiana kuhusiana na maswala mbalimbali ya kimaisha.

Sasa, kazi ya mfundisho ya neno la Mungu ni kutukusanya pamoja kama watoto wa kiume na wa kike wa familia moja mpaka kufikia mahala pa; Mungu mmoja, imani moja na ubatizo mmoja. Hiyo haitokei tu kwa kuokoka na kuanza kwenda kwenye kanisa fulani. Hayo ni matokeo ya kukaa kwenye fundisho la kanisa la mahala pamoja kwa mwendelezo.

Maeneo ambayo kanisa litatofautiana kiimani mfano ndoa, ustawi, afya ya kiungu na uponyaji, malezi ya watoto n.k, ni ujumbe kuwa mafundisho hayatoshelezi ama hayapo kabisa kwenye hilo eneo husika ndani ya kanisa hilo.

Ni lazima kama kanisa tuwe na usemi mmoja kiimani katika kila eneo linalogusa maisha yetu (holistic). Ukitaja kuhusiana na fundisho fulani, utagundua waamini wa kanisa la mahala pamoja wanauelewa mmoja. Sizungumzii maoni… FUNDISHO! Hicho kinaitwa umoja wa Imani.

iii. Umoja wa roho.

Kuna maeneo fulani ya kiimani ambayo kuna watu wapo nyuma kwenye kujifunza, wakati huo huo watu wengine kwenye eneo hilo hilo wameenda mbele. Hii ni kwa sababu kanisa la mahala pamoja si kama shule – muhula unaeleweka, mtaala umewekwa mahala pake, upimaji wa uelewa… kuna urasmi hivi. Kanisani, mtu anazaliwa upya saa yoyote na anajiunga na familia ya Imani. Kwa hiyo, siku zote kutakuwa na waamini wa matabaka tofauti ya kiimani kulingana na lini waliingia katika imani. Kuna sababu nyinginezo kadhaa za tofauti ya kiimani ndani ya kanisa la mahala pamoja. Si kusudio sana la kitabu hiki kuziendea na kuzijadili hizo kwa kina.

Ili hawa watu wote walioko kwenye matabaka mawili tofauti waweze kukaa ndani ya kanisa na ndani ya imani moja, inabidi umoja wa roho uwepo ndani ya kanisa.

Yaani, kutambua ya kwamba tuna tofautina katika uelewa wa fundisho (hapa simaanishi mafundisho ya ukengeufu, upotofu, uongo, nasaba na hadithi za wazee au mafundisho ya mashetani)… Hasha! Bali tuko kwenye

madaraja tofauti ya kuelewa jambo hilo. Utambuzi huo unakubali ya kwamba ndugu yangu katika Kristo ana nia njema ya kujifunza na kukua, hafanyi makusudi. Aina hii ya utambuzi hupelekea kukubali na kusisitiza juu ya umoja wetu kwa tendo la wokovu juu ya tofauti zetu za kiuelewa kwenye maeneo fulanifulani. Hutoa ruhusa, kwa upendo, kwa wengine kuelewa na kukua.

Kitakachowafunga pamoja ni kifungo kinachoitwa umoja wa roho, na kanisa linaloweza kufanya hivyo ni kanisa lenye mafundisho pekee. Nionyeshe kanisa lenye mafundisho nitakuonyesha kanisa lenye umoja wa roho.

Kwenye imani hii tuliyo nayo ndani ya Kristo, kuna mambo ya msingi ambayo hutuunganisha kwa pamoja. Kisha kuna mambo yasiyo ya msingi ambayo huwa tuna tofautiana kulingana na tafsiri, mapokeo, umahalashaji n.k

Mambo ya msingi ya kiimani ni kama vile: Uhalali wa Biblia kuwa ni Maandiko Matakatifu; Mungu mmoja wa pekee na wa kweli katika Utatu Mtakatifu; Uungu wa

Yesu Kristo; Uungu wa Roho Mtakatifu; Mwanadamu ni mwenye dhambi na kuna njia moja tu ya kumwokoa n.k

Mambo yasiyo ya msingi ya kiimani ni kama vile: Muda gani hasa ibada ifanyike; mpangilio wa ukaaji tuwapo ibadani na mambo yanayofanana na hayo.

Kanuni muhimu hapa ni: **Kwenye mambo ya msingi ya imani – UMOJA; Kwenye mambo yasiyo ya msingi ya imani – UHURU; Kwenye mambo yote ya imani – UPENDO.**

*In faith essentials –UNITY; In faith non-essentials – LIBERTY; In all things – LOVE.*

iv. Kuwa waalimu kwa waamini wachanga.

Watu walio na muda mwingi kwenye wokovu inatarajiwa ya kwamba wameutumia muda huo kujifunza kiasi cha kuwa walimu; Hivyo imewalazimu kuwa waalimu kwa wanaoanza kuukulia wokovu. Sio kila kundi linapaswa kufikiwa na mchungaji, sio kila somo linatakiuwa kufundishwa na mchungaji, sio kila kitu ataelezea mchungaji.

Kanisa lenye mafundisho linapaswa kuzaa watu ambao watakuwa waalimu. Neno la Mungu linawafinyanga waamini kwa kuwajengea uwezo wa kufundisha.

Kila rika ndani ya jamii ya waamini linapasa kufundisha kundi lililo chini yao. Wamama watu wazima wanapaswa kuwafundisha na kuwaelekeza mabinti.

Wababa watu wazima wanapaswa kuwafundisha vijana wa kiume.

Vijana wanatakiwa kuwafundisha vijana wadogo (teenagers). Neno la Mungu linatutarajia sote kuwa waalimu.

Ukosefu wa waamini walimu ni kiashiria ya kwamba kanisa lina changamoto eneo la mafundisho.

v. Tabia ya Rohoni.

Tabia ya rohoni inazungumziwa kwa upana katika kuhusiana na Mungu pamoja na kuhusiana na wanadamu. Kuna vitu kama waamini wenye mafundisho tunatakiwa kukua kuvizidi (outgrow).

Ndani ya kanisa linalokosa mafundisho utaona tabia za mwilini zikienea kama umbea, masengenyo, uongo n.k.

Watu wenye tabia ya mwilini hupenda kuwachukia watu wenye tabia ya rohoni na kuwaona wanajisikia sana. Watu wenye tabia za mwilini wanaona nidhamu za kiroho (kufunga, maombi, mafundisho, mikesha n.k) ni kama adhabu kwao. Watu wenye tabia ya mwilini huchoshwa na kukereka na mambo haya kwa urahisi.

Watu wenye tabia ya rohoni hupenda na hufurahia kufanya mambo ambayo yanawasogeza karibu na Mungu.

Ni kanisa lenye mafundisho pekee ndilo linaloweza kuinua watu wenye tabia ya rohoni.

vi. Tunda la Roho.

Kanisa la watu wenye mafundisho linadhihirika kutokana na watu wake kuonyesha uwepo wa tunda la Roho. Mahusiano miongoni mwa waamini yanapaswa kuendeshwa kwa misingi ya tunda la Roho, si kwa hisia au mazingira. Mwamini hapaswi kuwa kama homa – ina panda na kushuka. Anapaswa kuwa ni wa kutumainika na

kutabirika kitabia. Kimsingi, tunda la Roho ni tabia ya mtu aliyeko ndani ya Kristo.

Hii itatokea tu kwenye kanisa la mahala pamoja lililowekeza muda mwingi kwenye mafundisho.

Wagalatia 5:22-23, *"Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, Amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria."*

Tunda la Roho haliwezi kutokea pasipo kulifanyia kazi; Tunda la Roho halijitokezi tu jenyewe (automatically); Tunda la Roho si muujiza au karama – siyo kitu kinakutokea kwa ghafla tu bila hata wewe kujua na/ua kushiriki. Lakini mara nyingi, tunda la Roho hudhihirika pale ambapo unatakiwa kutenda kinyume nalo.

Mithali 19:11, *"Busara ya mtu huiahirisha hasira yake; Nayo ni fahari ya kusamehe makosa."*

Tunda la Roho lina kazi ya kukusaidia kutenda kinyume na hisia hasi kama vile hasira, huzuni na uchungu.

Kanisa lenye mafundisho lina nguvu ya kuzalisha watu ambao tunda la Roho ndani yao haliwezi kupuuzwa.

Na hiyo ndiyo ilikuwa mojawapo ya uti wa mgongo na nguvu za kanisa la Matendo ya Mitume.

vii. Karama za Roho katika kuhudumiana sisi kwa sisi.

Kanisa, kwa mfananisho wa mwili, limewekwa na kukusudiwa lijihudumie jenyewe. Litumie rasilimali zake za kiroho jenyewe. Kwa kutumia karama za roho, kanisa la mahala pamoja, lisipungukiwe msaada wa kiroho wa aina yoyote.

Ninaandika nikitambua kuna mjadala wa kitheolojia kuhusiana na karama, huduma na utendaji wa kiungu… wengine husema vimetolewa kwa ajili ya mwili wa Kristo, yaani, kanisa la ulimwengu wote (universal church). Hata hivyo, msimamo wangu ni kwamba vimetolewa kwa ajili ya kanisa la mahala pamoja. Nikimaanisha, utekelezaji wa ajenda zote za kanisa la ulimwengu wote hufanyika kwenye ngazi ya kanisa la amahala pamoja.

Unakumbuka ile orodha ya watu waliokusanyika kufanya maombi na ibada mbele za Bwana kwenye matendo ya Mitume? *"...manabii na walimu..."* Matendo ya Mitume 13:1. Umeona huo utumizi wa lugha kwa uwingi? Manabii – wengi (Zaidi ya mmoja); waalimu – wengi (Zaidi ya mmoja) na wote hawa ni washirika ndani ya kanisa la Antiokia. Hili ni moja ya kanisa la mfano. Kanisa lililoibadilisha dunia yake ya wakati huo kwa kutuma wahudumu wengi wa injili. Huwezi kutuma usichozalisha kwanza.

Ukienda mstari unafuatia utaona maelekezo ya Roho Mtakatifu, *"... nitengeeni Barnaba na Sauli kwa kazi ile niliyowaitia."* Matendo ta Mitume 13:2. Huwa ninauliza Sauli aliwekwa kundi gani kwenye ile orodha ya juu – manabii au waalimu… au kuna mitume, wainjilisti na wengineo kwenye kundi na kwa sababu ya muda (economy of time) hatukuambiwa? Mwandishi akatambua tukiona majina tutajiongeza? Inawezekana! Ndani ya kanisa moja, karama zote hizo.

Ili ujifunzaji uweze kutokea ni lazima mambo haya yazingatiwe.

- Muda.

Suala la kujifunza linahitaji kutengewa muda wa kutosha. Halitazaa matunda yapasayo kama litafanywa haraka haraka.

Matendo 17:11, *"Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo,* ***wakayachunguza maandiko kila siku****, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo,"*

Kama unataka kuweza jambo, inapaswa uwekeze muda mwingi katika kujfunza jambo hilo. Huwezi kuweka muda mchache kwenye ujifunzaji wa neno la Mungu na kutarajia mambo makubwa kutokea humo. Umeona mfano wa watu waungwana wa Beroya? Mara nyingi tunafahamu kipande cha kuyachunguza maandiko na hatujawahi kugundua ilikuwa ni kila siku. Hicho ni kipande cha muda! Biblia inaposema kila siku siyo kwamba inatia chumvi kupendezesha simulizi… ni kila siku!

Nehemia 8:1-3,*"Na watu wote wakakusanyika kama mtu mmoja katika uwanja uliokuwa mbele ya lango la maji; wakamwambia Ezra, mwandishi akilete kitabu cha torati ya Musa, BWANA aliyowaamuru Israeli. Naye Ezra, kuhani, akaileta torati mbele ya kusanyiko, la wanaume na wanawake, na wote walioweza kusikia na kufahamu, siku ya kwanza ya mwezi wa saba.* ***Akasoma humo*** *mbele ya uwanja uliokuwa ukikabili lango la maji,* ***tangu mapambazuko hata adhuhuri,*** *mbele ya hao wanawake na wanaume, na wale walioweza kufahamu; na masikio na masikio ya watu wote yakasikiliza kitabu cha torati."*

Angalia wakati wa urejesho, watu wote wamekusanyika kusikia neno likisomwa – siyo likihubiriwa. Muda uliotumika kwa ajili hiyo ni walau masaa sita (6), mapambazuko mpaka adhuhuri. Kuanzia saa 12 alfajiri mpaka saa 6 mchana. Huu ni uwekezaji mkubwa sana kulielekea neno la Mungu.

- Heshima.

Kujifunza kunaambatana na heshima. Huwezi kunufaika na maarifa usiyoyaheshimu. Ni lazima uheshimu Neno la Mungu linapofundishwa.

Nehemia 8:5-6, *"Ezra akakifunua kitabu machoni pa watu wote; (maana alikuwa juu ya watu wote); na hapo alipokifungua,* ***watu wote walisimama****; Ezra akamhimidi BWANA, Mungu Mkuu. Nao* ***watu wote wakaitika, Amina, Amina, pamoja na kuinua mikono yao; kisha wakainama vichwa vyao, wakamsujudu BWANA kifudifudi.****"*

Binafsi nimechagua kudhani ya kwamba huo siyo utaratibu iuliokuwa umewekwa wa kiibada (litrujia) bali ni mwitikio wa moyoni wa watu baada ya kulisikia neno likisomwa. Kwa wale wanaojua maswala ya kiitifaki unaweza kukubaliana na mimi heshima hizo zilizotolewa hapo hutolewa kwa mgeni rasmi/maalum au kwa mkuu aliyeko ndani ya nyumba saa hiyo.

Kusimama, kuinua mikono, kuinamisha vichwa na kusujudi – ni utoaji wa heshima kwa neno kama mamlaka kubwa.

Usipokuwa na heshima kwa maarifa, maarifa hayatakuheshimu wewe.

Heshima kwa Neno la Mungu hupelekea mtu/kanisa lenye nguvu kuwa na mwitikio wa kitofauti (mwitikio wa shukrani) kulieleka Neno la Mungu.

Ukionyesha heshima kwa Neno la Mungu halitakuacha kama ulivyo, hakika litakubadilisha!

Zaburi 119:18, *"Unifumbue macho yangu niyatazame maajabu yatokayo katika sheria yako."*

Kwenye sheria ya Bwana hausomi maandishi, hausomi machapisho, wala hadithi. Kwenye Neno kumejawa na maajabu. Unapolifungua usiliendee kwa ukawaida.

Kanisa la mahala pamoja lenye nguvu ni kanisa ambalo linajua ya kuwa kila mara Biblia inapofunguliwa ni muda wa kusikia na kutazama maajabu yatokayo katika sheria ya Bwana.

# SURA YA PILI:

# USHIRIKA WA KANISA LA MAHALA PAMOJA.

Kanisa lolote la mahala pamoja lenye nguvu lina hii sifa ya ushirika. Utagundua kuwa watu walioko kwenye kanisa lenye tabia hii sio watu wanaokuja na kuondoka tu, bali ni waamini ambao ni washirika pamoja. Ushirika wa aina hii sio kushirikiana tu bali wana hali ya mioyo yao kufungamanishwa pamoja.

Watu walioko ndani ya kanisa lenye tabia hii wanajiona kuwa wanafamilia wa kanisa hilo, hawapo kana kwamba wataondoka baada ya muda mfupi.

Baada tu ya kuokoka, Mungu alikusudia uwepo kwenye familia ambayo huko utalelewa na kukua kiimani pamoja na washirika wenzako. Ni kama jinsi mtoto mchanga anapozaliwa na haachwi tu akakue mahala popote bali analelewa kwenye muktadha wa familia.

Kwenye Ufalme wa Mungu, hairuhusiwi kuwa na watoto yatima wala watoto wa mtaani! Kanisa linapokumbatia washirika ambao wanahusiana nalo kwa namna ya *"kisanii"* hilo kanisa ni lazima litapoteza nguvu.

Waebrania 10:21, *"na kuwa na kuhani mkuu juu ya* ***nyumba ya Mungu****;"*

Mungu anataka kuhusiana na sisi kama watoto wa nyumba yake.

2 Samweli 7:12-13, *"Nawe siku zako zitakapotimia, ukalala na baba zako, nitainua mzao wako nyuma yako, atakayetoka viunoni mwako, nami nitaufanya imara ufalme wake. Yeye ndiye atakayejenga nyumba kwa Jina langu, nacho kiti cha enzi cha ufalme nitakifanya imara milele."*

Bwana Yesu ndiye utimilizwaji na ukamilifu wa unabii huo kwa Mfalme Daudi; na Bwana Yesu amekuja kujenga nyumba, familia au kaya. Yesu anapookoa mtu anamleta kwenye nyumba na anataka afundishwe, akue, ajengwe, na astawi ndani ya familia.

Hivyo kanisa ni zaidi ya jengo. Kanisa ni zaidi ya kusanyiko; Kanisa ni zaidi ya shughuli na ratiba za kikanisa… Kanisa ni familia!

**Dhana ya Ushirika wa kanisa la mahala pamoja (Membership & Fellowship) inakinzana na dhana mbili zifutazao:**

a) Utamaduni wa Utazamaji.

Tunaishi kwenye zama ambazo kuna fikra ya utazamaji imengia. Kanisa sio jumba la maonyesho wala utazamaji. Mchungaji sio mtumbuizaji ndani ya kanisa. Dhana hii ikiachwa iendelee inaondoa hali ya ushirika na kazi ya utumishi kuachwa ndani ya mabega ya watu wachache.

Kanisa lenye nguvu ni watu wanaojua kuwa wanatakiwa kuwajibika asilimia miamoja ndani ya kanisa la mahala pamoja.

b) Dhana ya fundisho lililopitiliza juu ya Ufalme wa Mungu.

Fundisho lolote lile likifundishwa kwa kupitiliza (extreme) ndani ya kanisa linaleta madhara. Hii haina maana kuwa fundisho la ufalme si la umuhimu bali linapaswa kufundishwa kwa ulinganifu na mafundisho mengine. Dhana hii imepanda fikra ndani ya watu kuwa maadamu ufalme wa Mungu ni mpana sana, basi mtu anao uwezo wa kuabudu mahala popote, kuabudu wakati wowote pasipo kuwa chini ya kiongozi (mchungaji) yeyote na wala hata kutokuwajibishwa na mchungaji yeyote.

Hii ilitokea kwenye nia njema kabisa ya kubomoa viambaza vilivyokuwa vimejengeka ndani ya mwili wa Kristo ili kuongeza ushirikiano, Lakini ikaenda umbali wa kuondoa hali ya uwajibikaji ndani ya waamini.

Kanisa lenye washirika wanaoamini kuwa wao ni wa "ufalme mpana wa Mungu" ambayo ni kweli kabisa, haimaanishi kuwa hawawezi tena kuwa wanafamilia wa kanisa la mahala pamoja. Kwenye ufalme wa Mungu

kuna utaratibu kuwa kila mshirika ni lazima alelewe kwenye “kaya fulani” ambayo ni kanisa la mahala pamoja.

Waefeso 2:19, *“Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu.”*

Yesu amekusudia kuwa wote aliowaokoa wasiwe wageni wala wapitaji bali wawe wenyeji nyumbani mwa Mungu; yaani kanis la maha pamoja.

Fikiria mtoto wangu wa kiume akatae kukaa chini ya maongozi na utaratibu ambao mimi na mama yake tumeuweka nyumbani. Nikimuhoji na kumuwajibisha aseme yeye ni Mtanzania?

Ni kweli ni Mtanzania… ni mtazania anayeishi nyumbani kwangu! Kimsingi, hata huo utanzania wake unahesabiwa kutokea kwangu.

**DHANA YA USHIRIKA WA KANISA LA MAHALA PAMOJA KI BIBLIA.**

Kazi ya kanisa la mahala pamoja ni kuthibitisha/kukubaliana na ukiri na ushuhuda wa mwamini. Kazi ya kanisa ni kuuthibitishia ulimwengu ya kwamba mtu fulani ameokoka. Imani ni swala binafsi baina ya mtu na Mungu; Pia imani ni swala la kijamii. Huwezi kujisemea tu, *"Nimeokoka… anajua Mungu na mimi ninajua!"* halafu ikaishia hapo. Si hivyo kwa imani hii ndani ya Kristo Yesu.

Kanisa linaweza vile vile kuthibitisha kuwa fulani hajaokoka. Sasa, kuna upana wa kifundisho hapa kuhusiana na mamlaka hii kubwa ya kanisa la mahala pamoja. Nitagusia mambo kadhaa kwa rejea ya kimaandiko.

Hii ni kuonyesha nguvu na mamlaka ambayo Bwana Yesu aliliachia kanisa la mahala pamoja.

Mathayo 18:15-17, *"Na ndugu yako akikukosa, enenda ukamwonye, wewe na yeye peke yenu; akikusikia, umempata nduguyo. La, kama hasikii, chukua pamoja*

*nawe tena mtu mmoja au wawili, ili kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu kila neno lithibitike. Na asipowasikiliza wao,* ***liambie kanisa pia, na awe kwako kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru.****"*

Kwa muktadha huu, mtoza ushuru haitajwi kama kazi au cheo. Unakumbuka Yesu alishutumiwa kuwa anakula na kushirikiana na watoza ushuru? Ni neno linalotumika kumaanisha, "wenye dhambi!" au watu waovu na waioamini.

Angalia maelezo ya Bwana Yesu mwenyewe, anazungumza kuhusu "ndugu". Yaani mwaminini mwenzako. Huu tunaita mchakato wa unidhamishaji ndani ya mwili wa Kristo. Hatua ya mwisho ni kuliambia kanisa. Kisha huyo ndugu akionekana kuwa mkaidi kwa kanisa, basi achukuliwe kama mtu asiye amini… mtenda dhambi… mtu ambaye hajaokoka.

Kanisa linaweza kufikia hilo hitimisho! Kwa mwenendo wa moyo usio na toba wa ndugu yetu, tumefikia hitimisho ya kwamba huyu ndugu inawezekana kumbe hata

hajaokoka… ndiyo tangazo linalotolewa na kanisa kwa umma.

Imani ni binafsi – wewe na Mungu…. Na kanisa!

Tusogee mbele kidogo na hii shule ya ushirika wa kanisa la mahala pamoja. Kuwa mshirika ni kuhesabika na kufahamika. Na hii inaweza kuwa na maana kadhaa mbele za Mungu:

i. Kiidadi.
ii. Kitaarifa.
iii. Kimaisha.

Matendo ya Mitume 2:41-42, *"Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile* ***wakaongezeka watu wapata elfu tatu****. Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katiak kuumega mkate, na katika kusali."*

Matendo 5:14, *"walioamini wakazidi* ***kuongezeka*** *kwa Bwana, wengi, wanaume na wanawake."*

Kwenye maandiko hayo ninataka uone mambo mahususi. Inaposema watu elfu tatu hii ni jambo mahususi (specific)

sana. Maana yake wanafahamika, wanahesabika na wanatambulika. Nani yumo na nani hayumo. Kusema idadi hiyo ya watu ni sawa na kuwatambua watu na kutowatambua watu fulani. Kwa idadi hiyo mahususi inaondoa dhana ya makisio au kudhania tu. Kama umo kwenye watu elfu tatu ni jambo linalofahamika kwako na kwetu.

Fikiria unakutana na baba wa familia asiyejua idadi ya watu wa nyumba yake. Baba asiye na uhakika kama "fulani" ni sehemu ya familia au si sehemu. Au unakutana na vijana wanaojitaja kuwa watu wa nyumba ya fulani na hali baba hatambui.

Kwa mfano huo na mafafanuzi ya awali, ninaruhusiwa kudhani ya kwamba inawezekana si tu idadi ya kuhesabika bali watu walikuwa na namba ya kuwatambulisha. Yaani, kati ya wale watu elfu tatu, mimi James Kalekwa ni nambari 2024. Ninawaza hivyo dhidi ya wazo la watu kusingizia ya kwamba wao ni sehemu ya wale elfu tatu na kumbe siyo.

Ninajua mtu anaweza kusema, mchungaji, hilo la kuwahesabu watu na kuwatambua kwa nambari linawezekana kwa makanisa yenye idadi chache ya watu… Mpenzi, ulichokisoma kwenye Mtaendo ya Mitume ni watu elfu tatu kwa siku moja! Kanisa linaongezeka tena na tena mpaka linaanza kuyatambua makundi yenye mahitaji maalum (rejea Matendo ya Mitume 6:1-6).

Kutokea kwenye uelewa huo, kuwa mshirika wa kanisa la mahala pamoja ni kuhesabiwa na kutambulika kwa nambari (au utaratibu mliojiwekea).

Matendo 11:19-21,24, *"Basi **wale waliotawanyika** kwa sababu ya ile dhiki iliyotukia kwa habari ya Stefano, **wakasafiri hata Foinike, na Kipro na Antiokia,** wasilihubiri lile neno ila kwa wayahudi peke yao. Lakini baadhi ya hao walikuwa watu wa Kipro na Kirene, nao walipofika Antiokia wakasema na wayahudi wa Kiyunani, wakihubiri habari njema za Bwana Yesu. Mkono wa Bwana ukawa pamoja nao, watu wengi wakaamini, wakamwelekea Bwana. Maana alikuwa mtu mwema*

*amejaa Roho Mtakatifu na Imani; watu wengi wakaongezeka upande wa Bwana."*

Hapa ninataka uone neno "wale waliotawanyika". Kwenye utumizi wa lugha hili ni neno mahususi… linamaanisha wanafahamika! "Wale" inatuondoa kwenye ufikiri wa "yeyote yule". Hapa kuna watu mahususi ambao tunawarejelea. Sasa, hao watu wanafahamika wako wapi – Foinike, Kipro na Antiokia. Wameaga kanisani… inawezekana. Wana mawasiliano kanisa walilotoka au wameunganisha kimawasiliano kanisa walilofikia na kanisa walilotokea… huenda. Vyovyote vile, lakini wanafahamika wako wapi!

Ushirika umegawanyika katika ngazi kuu mbili:

Matendo 2:46

*"Na siku zote kwa moyo mmoja* ***walidumu ndani ya hekalu****, wakimega mkate* ***nyumba kwa nyumba****, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe."*

i. Ushirika wa hekalu/ ushirika kwenye kusanyiko kubwa.

ii. Ushirika wa nyumba kwa nyumba/makusanyiko madogomadogo.

Mshirika yeyote ni lazima ahesabiwe kwenye ngazi zote mbili.

**Sababu za kuwa mshirika wa Kanisa la mahala pamoja:**

i. Kanisa linakuwa ni jukwaa la kukusanyika pamoja.

Waebrania 10:24-25, *"tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri; wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia."*

Kanisa ndio linakupa watu wa kukuweza kukusanyika pamoja nao. Ukilikatalia kanisa, basi umejikatalia watu wa kuweza kukusanyika nao. Huwezi kukusanyika peke yako. Biblia inasema *"kukusanyika pamoja!"*

Huwezi kukusanyika peke yako. Sehemu ambapo tunakutana ni kwenye muktadha wa kanisa la mahala

pamoja. Na ili kutii andiko hili inapaswa washirika kukusanyika kwenye kanisa kubwa na kanisa la ushirika wa nyumba kwa nyumba.

Kanisa la mahala pamoja linakufadhili kwa kukupa watu… jamaa ya imani… familia na ndugu wa kukusanyika nao!

ii. Kuweza kutimiza amri za kutendeana.

Kwenye neno la Mungu kuna amri zaidi ya hamsini zinazoagiza kutendeana.

Yakobo 5:16, *"Ungameni dhambi zenu* ***ninyi kwa ninyi,*** *na* ***kuombeana (ninyi kwa ninyi)****, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii."(Mkazo wa kwenye mabano ni tafsiri na nyongeza yangu binafsi)*

Sehemu ya kutekeleza maagizo ya "ninyi kwa ninyi"ni kwenye muktadha wa kanisa, mahala walipo waamini wenzako ili waweze kukuombea na uweze kuwaombea pia.

Kwenye mfululizo wa mafundisho kwa njia ya maandishi uitwao kuimarisha kanisa la mahala pamoja. Nimeandika kitabu kinaitwa **Ninyi kwa Ninyi:** *Amri za kutendeana miongoni mwa jamii ya waaminio.* Ambacho kitaifafanusha dhana hii kwa mapana na kina chake.

iii. Kanisa la mahala pamoja ni jukwaa la matumizi ya karama au vipawa.

1 Petro 4:10-11, *"kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama,* ***itumieni kwa kuhudumiana****; kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu."*

Karama alizotupatia Mungu sio kwa ajili yetu wenyewe, ni kwa ajili ya kuwahudumia wengine. Matumizi ya karama ni kwa ajili ya jukwaa linaitwa kanisa.

Sehemu pekee unaweza kunufaika na karama nyingi kwa wakati mmoja ni kanisani. Ukijitenga na kanisa maana yake umejitenga na karama za Mungu. Sehemu pekee unayoweka kuchochea karama ya Mugu iliyomo ndani mwako na kisha kuitumia kuwafaidia wengi ni ndani ya muktadha wa kanisa la mahala pamoja.

# SURA YA TATU: UTOAJI WA KUJIDHABIHU

Kanisa la mahala pamoja lenye nguvu ni kanisa ambalo linafahamu kuwa lina wajibu wa kutoa kwa kujidhabihu. Ni wajibu wa kanisa hili kutoa fedha, mali, ujuzi, uzoefu, muda, na maarifa kwa ajili ya kazi ya Bwana Yesu. Kanisa la mahala pamoja limebeba utambuzi ya kwamba kazi ya msalaba na matokeo yake iligharimu uhai wa Bwana Yesu kwa hiyo, itatugharimu kila kitu.

Vitu ambavyo Mungu amewabarikia watu wake kwavyo; kwanza ni kwa ajili ya kuujua na kuutambua wema wake lakini pia ni kwa ajili ya kuwezesha kazi yake. Hili ni jambo ambalo kila mwamini anapaswa kulijua.

Kanisa lolote la mahala pamoja ambalo lina nguvu, ni kanisa ambalo linaujua vyema wajibu wake wa kutoa kwa kujidhabihu.

Matendo 20:35, *"Katika mambo yote nimewaonyesha ya kuwa kwa kushika kazi hivi imewapasa kuwasaidia*

*wanyonge, na kuyakumbuka maneno ya Bwana Yesu, jinsi alivyosema mwenyewe, **Ni heri kutoa kuliko kupokea.**"*

Heri maana yake ni baraka. Kutokea hapo inajengwa kanuni muhimu sana… kutoa ni baraka!

Utoaji ni udhihirisho wa imani, ni namna ya kuidhihirisha imani yako. Namna unavyotoa inaonyesha namna unavyoamini. Kama unapata shida kwenye kutoa basi una shida ya imani na sio ya pesa. Kutoa kunaanzia moyoni na sio mfukoni.

## Madaraja matatu ya utoaji:

i. Utoaji kumuelekea Bwana.

ii. Utoaji kuielekea kazi ya Bwana.

iii. Utoaji kumuelekea mtumishi wa Bwana.

Kutoa kwenye aina moja ya daraja hakukuzuii kutoa kulielekea daraja moja au madaraja mengine.

### i. Utoaji kumuelekea Bwana

Sadaka ni jambo linaloanzia moyoni. Ni vizuri sana kukagua hali ya moyo kabla ya kutoa. Sadaka ni ujumbe ambao moyo unasema kuhusiana na imani yako.

Hivyo kila mara unapopeleka sadaka yako kwa Mungu, yeye haangalii kwanza sadaka bali anaangalia ujumbe wa moyo nyuma ya sadaka.

Baadhi jumbe ambazo Mungu anaweza kupokea kutokea kwenye sadaka ni kama vile;

- Ujumbe wa heshima.

Mithali 3:9, *"**Mheshimu** BWANA kwa kwa mali yako, na kwa malimbuko ya mazao yako yote."*

Unaweza kumheshimu ama kumdharau Bwana kwa mali yako. Utoaji ni kifaa cha kuonyesha heshima kwa Bwana na kwa utendaji wa kazi yake.

- Uchaji, hofu, ibada.

Unapotoa sadaka ni sehemu ya ibaada yako kwa Mungu.

Mwanzo 22:12, *"Akasema, usimnyoshee kijana mkono wako, wala usimtendee neno; kwa maana sasa ninajua ya kuwa **unamcha Mungu**, iwapo hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee."*

Kitu chenye uwezo wa kuukamata uchaji wa moyo wa mtu ni mali. Linapokuja swala la ibada mali ina uwezo ule

ule wa kuukamata moyo wa mtu kama Mungu anavyoweza kufanya. Ndiyo maana Bwana Yesu akifundisha aliiweka mali kwenye daraja la Mungu aliposema, "… huwezi kuwatumikia mabwana wawili..." Hao mabwana siyo Mungu na Shetani bali Mungu na mali!

- Tumaini au tegemeo.

Malaki 3:14, *"Mmesema, kumtumikia Mungu hakuna faida; na, Tumepata faida gani kwa kuyashika maagizo yake, na kwa kwenda kwa huzuni mbele za BWANA wa majeshi?"*

Hii ndiyo siri na fundisho kubwa nyuma ya sadaka iitwayo zaka/fungu la kumi. Ni namna ya kuonyesha utegemezi wa mtu binafsi kwa Mungu.

Iko hivi, kiasi cha fedha unachopata ndani ya muda fulani huwa hakikutoshi kuyaendesha maisha yako na kukutana na mahitaji yako na ya wale uwapendao- watu wa nyumbani mwako. Hakuna siku itafika utasema, nina vyote!

Sasa, kutokea kwenye rasilimali zisizokutosha, Mungu anataka umtolee sehemu ya kumi ili upungukiwe zaidi… Hii ni kinyume cha mantiki kabisa. Hata hivyo, aina hii ya utoaji inakulazimisha sasa umtegemee Mungu kwenye eneo hilo kama mpaji. Kwa sababu kutoka kwenye hazina ambayo haitoshi, Mungu ametaka nimtolee. Unaelewa?

Mungu akitaka umtegemee anakutegua kutokea kwenye kiasi cha fedha ambacho hakitoshi ili umtegemee Yeye. Husemi ninamtegemea Mungu kwa maneno ya midomo tu bali unasema kwa mali na fedha zako.

Kanisa la mahala pamoja lenye nguvu linawasilisha ujumbe huu wa utegemezi wao kwa Mungu kwa njia ya utoaji wa namna hii.

- Vipaumbele vya maisha.

Hagai 1:4, *"**Je! Huu ndio wakati** wa ninyi kukaa katika nyumba zenye mapambo ya mbao, iwapo nyumba hii inakaa hali ya kuharibika?"*

Hapa si kwamba Mungu ana ugomvi na watu wake kujenga nyumba nzuri na mapambo ya kupendeza. Swali

lipo kwenye “Huu ndiyo wakati?”. Ni swala la vipaumbele.

Usipokuwa na sehemu nzuri ya kufanyia ibada inaonyesha hali ya moyo wako. Namna unavyotoa kwa Mungu inaonyesha mpangilio wa vipaumbele vya maisha yako.

### ii. Utoaji kuielekea kazi ya Bwana.

Kuna wazo ninaliona likijirudia kwa mwonekano, maumbo tofauti kulingana na nyakati. Hata hivyo kusudi la wazo hilo ni moja – Mungu akae katikati ya watu. Awe Mungu kwao, nao wawe watu wake. Hilo wazo ni la ujenzi wa eneo la kimwili ambalo litakuwa mahali pa kukusanyikia baina ya Mungu na watu wake. Ninafanya uchambuzi mfupi sana wa awamu tatu za ujenzi wa nyumba ya Bwana:

- Ujenzi wa hema ya kukutania. (Sanctuary) – Kipindi cha jangwani.

Mungu alipotaka kuishi katikati ya watu wake kwa alama inayooeana katika mwili, alihitaji kujengewa kitu kinaitwa hema ya kukutania (Sanctuary).

Kutoka 35:4-5, *"Kisha Musa akanena na mkutano wote wa wana wa Israeli, akawaambia, Neno hili ndilo aliloliamuru BWANA;* ***mtu awaye yote aliye na moyo wa kupenda, ayalete matoleo; dhahabu, na fedha, na shaba****;"*

Wanaojenga mahala ambapo Bwana anaabudiwa ni wanufaika wa ibaada hiyo. Mungu hawezi kuinua mtu mwingine kukujengea mahala pa ibada yako mwenyewe.

Kutoka 36:6b-7, *"Basi watu wakazuiwa wasilete tena* ***kwani vile vitu walivyokuwa navyo vilikuwa vyatosha kwa kuifanya kazi hiyo yote, kisha vilizidi****."*

Ajabu na kweli ni kwamba watu hawa wa Mungu walitambua wajibu wao na waliitikia kwa tendo na kuzidi matarajio.

Nataka ufuatilie hili wazo endelevu vizuri ya kwamba wanaoijenga kazi ya Bwana ni wanufaika wa kazi hiyo husika.

- Ujenzi wa hekalu la Sulemani – Wakati Ufalme, nchi ya ahadi.

1 Nyakati 29:2-4, *"Basi kwa* ***uwezo wangu wote nimeiwekea akiba ya nyumba ya Mungu wangu****…."*

Unaona kuna akiba imewekwa hapa na mtu wa Mungu, mfalme Daudi, na nyumba yake kama mnufaika wa kwanza wa ibada itokayo hekaluni. Mnufaika wa ibada ndio mtoaji wa kwanza kuielekea kazi ya Mungu.

Mungu anataka mahali pa kuabudiwa pa kudumu. Daudi anaweka nia na anakusanya rasilimali za kutosha na kupitiliza ili kumjengea Bwana.

- Ujenzi wa hekalu la Sulemani – Wakati wa Urejesho kutoka uhamishoni.

Kwa faida ya uelewa tu, ni kwamba baada ya Mfalme Sulemani kutawala, taifa la Israeli liligawanyika vipande viwili chini ya ufalme wa mwanae, Rehoboamu. Ufalme wa Kaskazini (Isareli) chini ya Yeroboamu, makao yake makuu pakawa ni Samaria; Ufalme wa Kusini (Yuda) chini ya Rehoboamu, makao yake ikawa ni Yerusalemu… hawa baadaye walifahamika kama Wayahudi wakati ndugu zao wa Kaskazini wakaitwa Wasamaria.

Sasa, Samaria walitawanywa juu ya uso wan chi kwa sababu ya ibada ya sanamu. Kisha, Yuda nao walichukuliwa uhamishoni – Babeli kwa miaka sabini. Sasa, kurejea kutoka uhamishoni ndiyo huku ninakokuzungumzia hapa.

Kurejea kulifanyika kwa makundi makubwa matatu; kundi la kwanza liliongozwa na Zerubabeli; kundi la pili liliongozwa na Ezra na kundi la tatu liliongozwa na Nehemia. Jambo la kuvutia ni kwamba, Zerubabeli alishughulika na ujenzi wa madhabahu; Ezra alishughulika na sheria na taratibu za ibada (mimi huuita ujenzi wa watu kuilekea madhabahu) kisha Nehemia akashughulika na ujenzi wa kuta zilizokuwa zimebomolewa na hali za watu kijamii na maongozi.

Anayejenga ibada ni mnufaika mwenyewe wa ibaada. Kama ipo nafasi ya kumjengea Mungu jengo la ibada la heshima, basi ni vyema kila mshirika akawa sehemu ya kazi hiyo.

Hapa ndiyo kuna ile simulizi ya kitabu cha Hagai. Watu kutaka kujenga nyumba zao kabla ya nyumba ya Bwana.

Hagai 1:4, *"**Je! Huu ndio wakati** wa ninyi kukaa katika nyumba zenye mapambo ya mbao, iwapo nyumba hii inakaa hali ya kuharibika?"*

Angalia maelekezo yaliyofuatia baada ya hapo (Hagai 1:9)

- Pandeni milimani
- Mkalete miti
- Mkaijenge nyumba

Kwa ujumla wake utagundua wazo linabaki paleplae ya kuwa wajenzi wa madhabahu ya Bwana; mahala pa kukutanikana baina ya Mungu na watu wake ni wale wanufaika wa ibada hiyo.

Hapa Mungu anwaambia LIPENI GHARAMA!

### iii. Utoaji kumuelekea mtumishi wa Mungu.

Tunapotoa kumuelekea mtumishi wa Mungu tunakutana na mahitaji yake ya aina mbili ambayo kwanza ni mahitaji kuielekea huduma na pili ni mahitaji yake binafsi.

Gharama zozote zile amabazo mtumishi wa Mungu anazitoa sio kwa ajili yake mwenyewe au familia yake

bali ni kwa ajili ya kuhudumia maeneo mbalimbali ya maisha ya washirika wake. Na katikati ya huduma hizo zote basi yapo mahitaji kwa ajili ya huduma hizo.

Watumishi wengi wa Mungu wanaovutia ki maarifa na kimuonekano wa kiroho na kimwili, washirika wao ndio wamewekeza kwao kwa kuyahudumia mahitaji ya maisha yao. Ninakuasa, tunza mtumishi wenu. Tunza mhudumu wenu wa injili.

1 Wakorintho 9:6-14, *"Au je! Ni mimi peke yangu na Baranaba tusio na uwezo wa kutokufanya kazi?* ***Ni askari gani aendaye vitani wakati wo wote kwa gharama zake mwenyewe?*** *Ni nani apandaye mizabibu asiyekula katika matunda yake? Au ni nani achungaye kundi, asiykunywa katika maziwa ya kundi?".*

Kanisa la mahali pamoja lenye nguvu ni kanisa linalotambua wajibu wao wa msingi wa utoaji wa kujidhabihu kumuelekea mtumishi wa Mungu… ni kanisa linalojua kutunza askari wao ili anapoenda vitani, abaki vitani kiakili na kimwili.

## Dhana ya Upimaji wa Sadaka.

Marko 12:41-43, *“Naye akaketi kulielekea sanduku la hazina, akatazama jinsi mkutano watiavyo mapesa katika sanduku. Matajiri wengi wakatia mengi. Akaja mwanamke mmoja, mjane, maskini, akatia senti mbili, kiasi cha nusu pesa. Akawaita wanafunzi wake, akawaambia, Amin, nawaambia, Huyu mjane maskini ametia Zaidi kuliko wote wanaotia katika sanduku la hazina; “*

Yesu anawaita wanafunzi wake na kuwaonyesha ni kwa jinsi gani Yeye hupima utoaji wa sadaka kwa sababu ni kweli hupima! Kipimo cha sadaka ni uwiano wa kile unachotoa kwa kile ulichobakiza nyuma hapo ndipo unapata sadaka.

Kimsingi, kila mtu hutoa. Lakini kwa mujibu wa tathmini ya Bwana Yesu ni kwamba kuna watu huwa wametoa mabaki ya hazina; na kuna watu hutoa uzito wa hazina yao.

Ni vyema kanisa likajua ya kwamba Bwana Yesu analipima kwenye utoaji. Pili, ni vyema kutambua mizania ya Yesu kwenye utoaji wa sadaka. Kwa sababu

shughuli za kiroho huambatana na thawabu. Kwa hiyo, Yesu hutoa thawabu sawa na alivyopima mwenyewe.

Kanisa la mahala pamoja lenye nguvu, utaiona nguvu yake kwenye utoaji. Ikifika wakati wa kumtolea Bwana sadaka, ni wakati wao wa furaha, mashangilio na bubujiko. Siyo wakati wa unyonge, udhaifu na upweke. Kuna kitu wanajua kuhusu utoaji, namna ya utoaji,vipimo vya utoaji na yatokanayo na utoaji.

**Pande mbili pacha za muamala wa sadaka.**

Waebrania 7:8, *"Na **hapa** **wanadamu wapatikanao na kufa** hutwaa sehemu ya kumi; bali **huko** yeye **ashuhudiwaye kwamba yu hai.**"*

Sadaka zinapokelewa sehemu mbili kwa wakati mmoja, *"hapa"* kwa maana ya wanadamu wa kawaida wenye mwili na *"huko"* ambako ni Bwana Yesu mwenyewe.

Inapopokelewa na mwanadamu inachukuliwa kama pesa lakini mbinguni inaenda kama moyo wa ibada, uchaji, shukrani na hofu yako kwa Mungu.

Matendo 5:1-3, *"Lakini mtu mmoja jina lake Anania, pamoja na Safira mkewe, aliuza mali, akazuia kwa siri*

*sehemu ya thamani yake, mkewe naye akijua haya, akaleta fungu akaliweka miguuni pa mitume. Petro akasema, Anania, kwa nini shetani amekujaza moyo wako* ***kumwambia uongo Roho*** *Mtakatifu, na kuzuia kwa siri sehemu ya thamani ya kiwanja?"*

Unaona shule ya sadaka kwenye andiko hilo? Sadaka imetolewa kuwelekea Mungu na kazi yake. Kwa hapa duniani iliwekwa kwenye miguu ya mitume, na huko aliipokea Mungu mwenyewe. Unaona upimaji wa sadaka unafanyika hapo? Amemdanganya Roho Mtakatifu. Inawezekana lilikuwa ni *"fungu nono"* tukizungumza kibinadamu… lakini kwa vipimo vya mpokeaji sadaka, ni uongo! Ilipaswa kuwa zaidi ya hapo.

Kanisa ni mahala pa kupewa heshima na sadaka zote inabidi zitolewe kama jinsi ambavyo inatakiwa hali washirika wakiwa na ufahamu ya kuwa sadaka zote zinapokelewa pande mbili.

# SURA YA NNE:

# UTARATIBU NA NIDHAMU YA WAAMINI.

Kwa kadiri ambavyo mkazo wa kinidhamu na unavyopunguzwa ndani ya kanisa ndivyo ambavyo kanisa linazidi kupungukiwa nguvu. Kama kanisa ni lazima tujifunze suala la nidhamu na utaratibu wa kanisa kwa mkazo wake. Pamoja na neema na rehema tunazozipata kwa Bwana Yesu, nimefikia kwenye utambuzi, kupitia Maandiko Mtakatifu ya kwamba kanisa siyo sehemu ya hovyo hovyo! Ni sehemu ya nidhamu… tena nidhamu ya hali ya juu sana.

## DHANA YA NIDHAMU YA KANISA

Dhana hii inaanza kwa kujua kwanza kanisa ni nini. Kanisa ni kundi dogo lililoitwa kutoka ulimwenguni ili litengwe mbali na dunia. Kutengwa ni kuwekwa pembeni kwa ajili ya matumizi au kazi maalumu. Kwa lugha ya kibiblia hii ndiyo maana ya WAKFU!

Kanisa lina kazi ya kuudhihirisha utukufu wa Mungu ambao hauwezi kuonekana duniani. Kwa msingi huo basi, kanisa halipaswi kufanana na dunia. Na ni kanuni kuwa huwezi kubadilisha kitu ambacho unafanana nacho. Inabidi utofautiane nacho kwanza ndipo uweze kukibadilisha.

Kanisa limeitwa litembee tofauti na dunia, lienende tofauti na dunia, litende tofauti na dunia kwenye nyanja zote za kimaisha.

1 Wakorintho 9:19-23, *"Maana, ingawa nimekuwa huru kwa watu wote, nalijifanya mtumwa wa wote, ili nipate watu wengi Zaidi. Nalikuwa kama myahudi kwa wayahudi, ili niwapate wayahudi; kwa wale walio chini ya sheria, nalikuwa kama chini ya sheria, (ingawa mimi mwenyewe si chini ya sheria), ili niwapate walio chini ya sheria. Kwa wale wasio na sheria nalikuwa kama sina sheria (si kwamba sina sheria mbele za Mungu, bali mwenye sheria mbele za Kristo), ili niwapate hao wasio na sheria. Kwa wanyonge nalikuwa mnyonge, ili niwapate wanyonge. Nimekuwa hali zote kwa watu wote, ili kwa njia zote nipate kuwaokoa watu. Nami nafanya*

*mambo yote kwa ajili ya Injili ili kuishiriki pamoja na wengine."*

Mara nyingi watu wanataka kuwa kama dunia pasipo kuwa na lengo. Lakini mtume Paulo alilazimika kuwa kama watu wa duniani ili awaokoe wote kupitia kuwashirikisha Injili.

Kanisa limeitwa kutofautiana na dunia, na kama italilazimu kanisa kufanana na dunia basi na iwe ni kwa ajili ya kuibadilisha hiyo dunia.

Nidhamu ni upekee/utofauti wa kanisa, ile hali ya kutengwa na kuwekwa pembeni kwa kanisa ili lizae matunda ndiyo nidhamu yenyewe ya kanisa.

Kanisa linapaswa kuulinda kwa nguvu zote upekee wake kwa sababu huo ndio utakaosaidia kwenye kuibadilisha dunia.

1 Wakorintho 5:1-4, *"Yakini habari imeenea ya kuwa kwenu ipo zinaa, na zinaa ya namna isiyokuwako hata katika Mataifa, kwamba mtu awe na mke wa babaye. Nanyi mwajivuna, wala hamkusikitika, ili kwamba aondolewe miongoni mwenu huyo aliyetenda jambo hilo.*

*Kwa maana kweli, nisipokuwapo kwa mwili, lakini nikiwapo kwa roho, mimi mwenyewe nimekwisha kumhukumu yeye aliyetenda jambo hilo, kana kwamba nikiwepo."*

Kanisa limepewa mamlaka ya kuikemea dhambi na hata kumkatilia mbali na kanisa huyo ndugu anayefanya dhambi.

Kanisa halipaswi kuchukuliana, kuvumilia na kujivunia uwepo wa mtindo wa maisha ya dhambi.

Wagalatia 6:1, *"Ndugu zangu, mtu akighafilika katika kosa lo lote, ninyi mlio wa Roho mrejezeni upya mtu kama huyo kwa roho ya upole, ukijiangalia nafsi yako usije ukajaribiwa wewe mwenyewe."*

Moja ya kitu kanisa linatakiwa kufanya ni kumuwahi kwa haraka mtu aliyetenda dhambi kwa kumrejeza kwa sababu analichafua kanisa liliooshwa kwa damu ya thamani sana.

Hebu nikuonyeshe maandiko kadhaa hapa kasha tufafanushe kutokea hapo na kujenga mtiririko wa wazo la nidhamu ya kanisa.

2 Wathesalonike 3:6, *"Ndugu, twawaagiza katika jina la Bwana Yesu Kristo, jitengeni nafsi zenu na kila ndugu aendaye bila utaratibu, wala si kwa kufuata mapokeo mliyoyapokea kwetu."*

1 Timotheo 1:20, *"Katika hao wamo Himenayo na Iskanda, ambao nimempa shetani watu hao, ili wafundishwe wasimtukane Mungu."*

1 Timotheo 5:20, *"Wale wadumuo kutenda dhambi uwakemee mbele ya wote, ili na wengine waogope."*

Kuendelea kuishi kwenye dhambi ni kama kansa, ikiachwa ina tabia ya kusambaa kwenye kiungo kingine. Na kama isiposhughulikiwa kabisa inasambaa kwenye mwili wote na mwisho wa siku inapelekea mauti.

Lengo la kushughulikia dhambi ndani ya kanisa sio kujivuna ama kuwaonyesha wanaoishi kwenye dhambi kuwa wao ni wabaya sana wakilinganishwa na "sisi"; Lengo siyo kuwadhalilisha na kujiinua "sisi". Lengo ni kuwasaidia wao ili watubu na kulilinda kanisa la Bwana Yesu. Nia ya kutekeleza fundisho la nidhamu kwenye

kanisa la mahala pamoja inapaswa kuwa safi na inayoongozwa na moyo wa Baba.

Dhambi zinaweza kufanyika sirini na hadharani. Dawa ya dhambi zinazomtesa mtu sirini ni kutafuta mwamini mkomavu na kumuungamia dhambi hizo, kwa mujibu wa neno la Mungu.

Dhambi ya hadharani ni ile inayogusa mwenendo/ushuhuda wa hadhara wa maisha ya mwamini kibinafsi kisha, kwa kanuni ya kuambatana (law of association) italiathiri na kanisa lote. Hatujaitwa kuwa watakatifu sirini peke yake, bali ni pamoja na kuwa watakatifu katika mwenendo na vile tunavyoonekaa nje mbele ya watu wa mataifa.

1 Petro 1:15, *“bali kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote;”*

Waebrania 13:18, *“Tuombeeni; maana tunaamini kwamba tuna dhamiri njema, tukitaka kuwa na mwenendo mwema katika mambo yote.”*

1 Petro 3:16, *"Nanyi mwe na dhamiri njema, ili katika neno lile mnalosingiziwa, watahayarishwe wale wautukanao mwenendo wenu mwema katika Kristo."*

1 Petro 3:1, *"Kadhalika ninyi wake, watiini waume zenu; kusudi, ikiwa wako wasioliamini Neno, wavutwe kwa mwenendo wa wake zao, pasipo lile Neno;"*

2 Petro 3:11, *"Basi, kwa kuwa vitu hivi vyote vitafumuliwa hivyo, imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mtakatifu na utauwa,"*

Tito 2:3, *"Vivyo hivyo na wazee wa kike wawe na mwenendo wa utakatifu; wasiwe wasingiziaji, wasiwe wenye kutumia mvinyo nyingi, bali wafundishao mema;"*

Kwa msingi huo wa neno la Mungu, unaweza kufikia kwenye hitimisho ya kwamba mwenendo ni ushuhuda wa muhimu sana toka kwa mwamini na kanisa kwenda kwa mataifa.

## Nani ananufaika na suala la nidhamu na utaratibu?

i. Mtu aliyeanguka dhambini.

Lengo la nidhamu na utaratibu wa kanisa ni kwa ajili ya kumsaidia aone ameanguka dhambini na arudi kundini. Kwenye fudisho la Bwana Yesu kuhusu nidhamu ndani ya jamaa ya waaminio anasisitiza "kumpata nduguyo" na anaambatanisha hali ya furaha ikiwa lengo hilo litafikiwa. Anaenda mbele zaidi kuonyesha ya kwamba ikiwa lengo halitafikiwa, basi itafutwe namna kama kukata rufaa hivi ili kulazimisha lengo hilo lifikiwe… kumpata ndugu! (Mathayo 18:15-20)

ii. Kanisa.

Maisha ya kukosa utaratibu yanaliumiza sana kanisa kwa sababu yananyonya nguvu kutokea kwenye kanisa. Huzalisha hali ya huzuni na maumivu ndani ya waamini. Kanisa linaposhughulikia mambo ya kinidhamu na utaratibu ni kwa ajili ya kuliponya kanisa. Kuliponya kanisa lisiendelee kuugulia maumivu; kuliponya kanisa kwa kuzuilia hali hiyo ya dhambi isisambae na kuenea ndani ya kanisa; kuliponya kanisa kwa kuulinda ushuhuda wake kwao walio nje.

Namna mbili za kulinufainisha kanisa na siri hii ya nidhamu ni kwa kutumia maonyo ya jumla kupitia mafundisho ya neno la Mungu. Pili, ni maonyo mahususi kwa njia ya kutaja majina na tukio husika (kwanza sirini kisha inapobidi, hadharani).

iii. Jamii inayolizunguka kanisa.

Maadamu kanisa limeitwa kuifundisha dunia, basi linapaswa sana kuuchunga mwenendo wake kwa ajili ya jamii ya watu wanaolizunguka kanisa wavutwe na mwenendo mwema wa kanisa.

Namna ya kuiponya jamii ni kwa kuliponya kwanza kanisa. Umewahi kusikia watu wa nje ya kanisa wakisema, *"Kama hivi ndiyo kuokoa, basi mimi nimeokoka sana!"* hapo wakirejelea aina fulani ya mwenendo wa mwamini. Unaona, kuna wakati ambao mwenendo wetu unazuilia sana mafundisho yetu kusikika. Sauti ya mwenendo inapaa sana kuliko ya mahubiri!

## Kwa nini tuonyeshe usimamizi wa nidhamu ya kanisa?

i. Kwa ajili ya kuonyesha upendo.

Ufunuo 3:19, *"Wote niwapendao mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidi, ukatubu."*

Mojawapo ya kuonyesha upendo ni kupitia kuwajibishana kama ndugu. Na ndicho ambacho Mungu hufanya – hupenda sana kiasi cha kuonya. Ukiona unaenenda kwenye mwenendo mbaya na hakuna mtu anakuonya na kukuwajibisha ndani ya kanisa wakati mwenendo wako unajulikana – *mpendwa, hupendwi!*

ii. Kwa ajili ya uponyaji.

2 Wathesalonike 2:15, *"Basi, ndugu, simamaeni imara, mkayashike mapokeo mliyofundishwa, ama kwa maneno, ama kwa waraka wetu."*

Kuna urejesho na uponyaji hutokea kwa njia hii ya nidhamu ya kanisa.

**Kuhusu Mwandishi:**
Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

**Kuhusu New Vine Church:**
Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

**Mawasiliano na Mwandishi:**



NEW VINE CHURCH | Dodoma



New Vine Church limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa *(Mathayo 5:13 -14/Yoeli 2:2 - 11).*

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz



**Mahali tulipo:** Swaswa mkabala na geti la Waziri Mkuu, Dodoma mjini.

## Ratiba za Ibada

**Alhamisi** Saa 11:15 jioni - saa 12:15 jioni

**Jumapili** Saa 3:00 asubuhi - saa 6:30 mchana

nvc_dodoma   +255 754 917 764

# KUHUSU MWANDISHI



James Kalekwa ni amemwamini Yesu kuwa BWANA na Mwokozi wa maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma


pastorjameskalekwa

+255 754 917 764

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

MchungajiJK

+255 754 917 764